



TANGAZO LA KAZI KWA NAFASI YA RIGGER

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi, uendeshaji, na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima Uganda mpaka Chongoleani Tanzania ambako kutajengwa gati na kituo cha kupakia mafuta ghafi karibu na bandari ya Tanga.

BESIX Ballast Nedam (BBN) Limited, ni MKANDARASI anayehusika kwenye mambo ya uhandisi, ununuzi na ujenzi wa gati na kituo cha kupakia mafuta ghafi ya mradi wa EACOP. BBN inawatangazia wazawa wa kata ya Chongoleani kuomba nafasi ya kazi ya Rigger. (Msaidizi katika Mashine za Ushushaji na Upakiaji Mizigo)

Nafasi za kazi – 5

Mradi	EACOP – Jetty & Loading Out Facility
Muajiri	BESIX Ballast Nedam Limited (BBN)
Mahali pakazi	Tanga
Nafasi ya kazi	Rigger
Mkuu wa Idara:	Meneja Ujenzi
Kipindi cha kazi	December 2023 – July 2025

Dhumuni la kazi

Jukumu kuu la Rigger ni kusaidia katika kuhamisha vitu vizito au mashine katika maeneo yanayotakiwa bila kusababisha uharibifu wa mzigo au mali inayosafirishwa au watu. Hii inajumuisha unyanyuaji na uhamishaji wa vifaa, kwakutumia mashine au visaidizi vingine huku ukizingatia kanuni na taratibu za usalama.

Majukumu ya kazi

- Kupangilia, kusawazisha na kutia nanga mashine.
- Kuweka mizigo sehemu ya kunyanyulia ili kutoa msaada au kutayarisha mzigo kwa kusogeza na kutumia mikono au zana.
- Kuhakikisha kuwa vifaa vya kubebea mizigo vinatenganishwa na kuhifadhiwa vizuri baada ya matumizi.
- Kufanya majaribio kwenye vifaa vya kubebea mizigo mara kwa mara ili kuhakikisha usalama na uaminifu.
- Kuwasiliana na wafanyakazi wanaohusika katika mchakato wa kupandisha na kupokea mizigo, kuhakikisha usalama wa wafanyakazi na vifaa.
- Kuhakikisha kazi yote imekamilika kwa usalama.
- Kufuata kanuni na tahadhari za usalama
- Kusimamia mchakato wa kufungua, kusafisha, na kuhifadhi vifaa vyovyote vya kubebea mizigo au mashine zilizotumika.



Sifa za muombaji.

Muombaji awe na sifa zifuatazo

- Angalau Elimu ya Shule ya Sekondari na mafunzo maalum katika uinujaji wa vitu vizito.
- Cheti cha mafunzo kutoka Taasisi ya Vifaa na Teknolojia nzito (IHET) ni muhimu.
- Uzoefu hasa kwa kazi za baharini.
- Utimamu wa mwili na lazima awe na uwezo wa kuinua na kubeba mizigo nzito.
- Uwezo wa kuwasiliana na kufanya kazi kwa umoja.
- Kujali usalama kwa kuepuka hatari zote zinazoonekana.

Vigezo na taratibu kwa waombaji

- Awe raia wa Tanzania
- Umri kuanzia miaka kumi na nane (18) na kuendelea.
- Awe mzawa wa kata ya Chongoleani
- Asiwe na rekodi ya uhalifu
- Barua ya maombi ya kazi ikionyesha anuani pamoja na namba ya simu ya muombaji.

Jinsi ya kutuma maombi:

Anuani kwaajili ya maombi ya kazi ni: **Meneja Mradi, BESIX Ballast Nedam Ltd. TANGA.** Maombi yote yatapokelewa kupitia ofisi ya kata ya Chongoleani au barua pepe jobs@bbnltd.co.tz na mwisho wa kupokea maombi haya ni 20 Desemba 2023.

Kwa maswali/maelekezo;- +255 747 958 460 (ndani ya muda wa kazi, saa 1:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni, Jumatatu hadi Jumamosi)

ZINGATIA. Kwa nafasi hii, waombaji kutoka maeneo mengine ya Tanzania hawatakiwi kupiga muhuri barua zao za maombi katika Ofisi ya Kata ya Chongoleani, Ni wazawa wa kata ya Chongoleani pekee wanaostahili kufanya hivyo.

HAKUNA AJIRA MLANGONI!!! USITOE HELA KUPATA KAZI!!!

TAMBUA KUWA, endapo hatutawasiliana na wewe wiki mbili baada ya tarehe ya mwisho ya tangazo hili, maombi yako yatakuwa hayajafanikiwa.